

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Nukushi: 028 270 0211
Baruapepe: acltanga@ardhi.go.tz



Kamishna wa Ardhi Msaidizi,
Mkoa wa Tanga,
S.L.P. 5058,
Tanga

Tafadhali unapojibu taja:

Kumb. Na. LD/TA/GF/035/11

Mkurugenzi Mkuu,
Tanzania Investment Centre,
S.L.P 938,
Dar es Salaam.



26/08/2020

**YAH: MALALAMIKO YA FIDIA YA MASHAMBA YA WANANCHI WA KATA YA
MTIMBWANI NA KWALE WILAYANI MKINGA.**

Rejea barua yenye **Kumb. Na. WV/K/MK VOL.124/6/2020** ya tarehe 24/06/2020 (Nakala ya
kivuli imeambatanishwa kwa rejea).

Hii ni kukufahamisha kuwa tumepokea malalamiko toka kwa wananchi wa Kata ya Mtimbwan
na Kwale Wilayani Mkinga wakiilalamikia Kampuni ya kigeni toka china ya *Hengya Cement*
Tanzania-Tanga kuchukua maeneo yao ya mashamba waliyokuwa wanayamiliki kiasili bila
kulipa fidia kwa mujibu wa sheria. Aidha, kumbukumbu zilizopo kwenye ofisi ya Mkurugenzi
Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga zinaonesha kuwa Kampuni hiyo imewalipa
fidia baadhi ya wananchi waliochukuliwa maeneo yao kwa ajili ya uwekezaji na baadhi ya
wananchi hawajalipwa fidia hiyo hadi sasa.

Fidia inayolalamikiwa na wananchi hao ni ile inayotokana na maeneo yaliyoongezwa kwenye
mradi, maeneo ya makaburi yaliyopo kwenye mradi, kutokulipwa fidia kwa mazao aina ya
mihogo ndani ya eneo la mradi, maeneo yaliyokuwa ndani ya mradi na hayakulipwa fidia na
mapunjo ya mazao na Ardhi yaliyopo ndani ya eneo la mradi. Kumbukumbu zinaendelea
kuonyesha kuwa jumla ya fidia inayolalamikiwa na wananchi hao ni **Tshs. 347,150,012.63** kwa
wananchi wanaokadiriwa kufikia takribani **142**. Hii ni kinyume na Sheria ya Ardhi Na. 4 ya
mwaka 1999 kifungu cha **3(g)**.

Kwa kuwa Kampuni hii ipo kwenye orodha ya Kampuni zinazosimamiwa na "*Tanzania*
Investment Centre-TIC" na kwa barua hii tunawasilisha madai yao kwenu ili wananchi hao
waliochukuliwa maeneo yao kwa ajili ya uwekezaji waweze kulipwa kwa wakati na wapate haki
yao stahili kwa mujibu wa Sheria.

Gwakisa T.
Kamishna wa Ardhi Msaidizi

Nakala: Katibu Mkuu,
40477 Dodoma

Kamishna wa Ardhi,
40477 Dodoma

Katibu wa Mhe. Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
40477 Dodoma